Together for girls

STRENGTH IN NUMBERS

Kwa kutumia taarifa kama mwongozo wetu, ushirika wetu wa Together for Girls (TfG), "Pamoja kwa Ajili ya Wasichana" kwa Kiswahili, unalenga kuongeza uelewa, kuhamasisha ufumbuzi wa matatizo unaozingatia ushaidi na kuratibu mipango ya kutokomeza ukatili dhidi ya wasichana na wavulana, kwa kutilia mkazo zaidi kwa wasichana.

Kwa kuanzishwa 2009, TfG ni ushirika kati ya serikali za kitaifa, mashirika ya Umoja wa Mataifa na mashirika katika sekta binafsi, unaofanya kazi pamoja katika kupambana na ukatili dhidi ya watoto ("VAC", kifupisho cha Kiingereza) na ukatili thidi ya wanawake ("VAW", kifupisho cha Kiingereza). Tunaleta pamoja sekta na wadau mbalimbali katika mbinu ya pamoja ya kupambana na kutafuta ufumbuzi wa ukatili.

Tunaweka mkazo zaidi kwa wasichana walio balehe kwa sababu mara nyingi hawaonekani ama hawathaminiwi katika uandaaji wa sera na mipango ya kutokomeza VAC na VAW.

Pia tunatambua kuwa wavulana nao hufanyiwa ukatilii wa kijinsia, na hivyo kujihusisha nao ni suala la muhimu sana sio tu kwa sababu haki zao na ustawi wao ni vya muhimu, bali pia kwa sababu wanalo jukumu muhimu katika kuvunja mzunguko wa ukatili.

Ushahidi uko wazi: Kuna nguvu katika idadi. Ni kwa kufanya kazi pamoja tu (na kwa kuhakikisha hatua pana ya mabadiliko ya jinsia) ndipo tunaweza kuvunja mzunguko uliokithiri kwa muda mrefu wa ukatili na kutengeneza ulimwengu salama na wenye usawa kwa watu wote.

WASHIRIKA

Canada · USAID · unicef · World Health Organization · Pan American Health Organization · UNAIDS · UN WOMEN · UNFPA · VIOLENCE AGAINST CHILDREN · End Violence Against Children · BD · CDC Foundation · cummins partners

TAARIFA. HATUA. UTETEZI.

Kuvunja mzunguko wa ukatili.

Washirika wa TfG ni viongozi wa kidunia katika maendeleo, kukinga na kutatua masuala ya ukatili, na kila mmoja huchangia utaalam na ujuzi wa pekee kuimarisha matokeo ya pamoja katika ngazi za kitaifa na kimataifa. Nguzo tatu za mbinu yetu zinajumisha:

TAARIFA

Tafiti za kitaifa zinazohusu ukatili dhidi ya watoto ("VACS", kifupisho cha Kiingereza), zinazoongozwa na Vituo vya Kimarekani Vinavyoshughulikia Udhibiti wa Magonjwa na Utoaji wa Kinga ("CDC", kifupisho cha Kiingereza), kama sehemu ya ushirika wa Together for Girls, zinatunza kumbukumbu kuhusu ukubwa, asili na matokeo ya ukatili wa kimwili, kihisia na kingono. VACS inachunguza ukatili dhidi ya wasichana na wavulana, ikitoa taarifa muhimu kwa viongozi wa serikali, jamii, asasi za kiraia na wafadhili.

HATUA

Ikiongozwa na serikali za kitaifa na UNICEF, nguzo hii hujikita zaidi kwenye uratibu wa sera zinazozingatia uhalisia na hatua za kimipango kukabiliana na matatizo yaliyobainika kupitia tafiti zilizofanyika. Hatua za kuchukua hujumuisha marekebisho ya sera, maboresho ya huduma kwa wasichana na wavulana waliofanyiwa ukatili na mipango ya kukinga ukatili usitokee.

UTETEZI

Ushirika wa Together for Girls umezindua jitiada ya kimataifa ya utetezi na uhamasishaji wa umma itakayoliwekea maanani tatizo la ukatili na kuhamasisha ufumbuzi unaozingatia ushaidi. Kupitia shuguli zetu za mawasiliano, tunatoa jukwaa kwa waanga wa ukatili, vijana na watetezi kushirikishana mikasa yao, na kuungana pamoja kuongoza mabadiliko katika jamii zao na kimataifa.

TAARIFA

Kwa sasa ushirika wetu uko hai katika **nchi zaidi ya 20** katika Afrika, Asia, Amerika ya Kusini, Karabia na Ulaya Mashariki. VACS imeweza kutengeneza taarifa kwa takriban **10% ya idadi ya watu chini ya miaka 25 duniani**, zinazosaidia kukuza uelewa na sera kuhusu VAC na VAW. Taarifa muhimu zitokanazo na Tafiti za Kitaifa Zinazohusu Ukatili Dhidi ya Watoto na Vijana ("VACS", kifupisho cha Kiingereza) zinajumuisha:

UKATILI WA KINGONO KABLA YA UMRI WA MIAKA 18 KATIKA NCHI ZENYE USHIRIKA WA TFG

- Katika nchi nyingi, zaidi ya 25% ya tendo la ngono kwa mara ya kwanza kwa wasichana lilikuwa la kulazimishwa.
- Ukatili dhidi ya wasichana unaongeza hatari ya maambukizi ya VVU (Virusi Vya Ukimwi), mimba zisizotarajiwa, matumizi ya vileo, kujiua na msongo wa mawazo.
- Ukatili dhidi ya wavulana huongeza hatari ya maambukizi ya VVU, matumizi ya vileo, msongo wa mawazo, ngono isiyo salama na baadae husababisha ukatili dhidi ya rafiki wa mwandani.



HATUA

- Kufikia leo, **nchi saba** zimeshaandaa ufumbuzi jumuishi katika sekta mbalimbali.
- Serikali ya Tanzania, kwa msaada wa UNICEF na serikali ya Kanada, imeweza kupanua timu za ulinzi wa watoto kitaifa katika mamlaka 47 za Serikali za Mitaa zilizowafikia zaidi ya watoto 700,000.
- Ili kutatafutia ufumbuzi matokeo ya utafiti kuhusu ukatili majumbani, na kwa msaada wa UNICEF na serikali ya Kanada, Cambodia ilitengeneza mbinu mkakati ya kitaifa kuhusu malezi bora ili kukinga kutokea kwa ukatili na matengano ya familia yasiyo ya lazima.
- Washirika wa serikali ya Malawi, kwa msaada wa UNICEF, ilitoa mafunzo kwa watoto zaidi ya 21,000 (75% wakiwa wasichana) kuwawezesha kujilinda na kujitetea. Takwimu zinaonyesha kuwa hatari ya kubakwa kwa wasichana imepungua kwa karibu ya 50%.
- Katika mwaka 2016, chini ya uongozi wa Shirika la Afya Duniani ("WHO", kifupisho cha Kiingereza), washirika wa TFG walishirikiana na mashirika mengine kutengeneza INSPIRE: Mbinu Saba za Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Watoto. INSPIRE inajumuisha baadhi ya mbinu zinazozingatia ushaidi nzuri uliopo na zilizo na uwezekano mkubwa wa kupunguza ukatili dhidi ya watoto, na ndio mwongozo wa jitihada za kitaifa.

UTETEZI

- Mnamo mwaka 2013, TFG ilizindua *Salama* ("Safe" kwa Kiingereza), jarida la kwanza la kidigitali linaloelezea watu, mashirika na nchi zinazofanya kazi za kila siku kuvunja mzunguko wa ukatili unao waathiri watoto, vijana na wanawake.
- Mnamo mwaka 2016, TFG ilianzisha kampeni Kila Saa Inayopita Ni Muhimu (Every Hour Matters, "EHM" kwa Kiingereza) ili kuongeza ulewa juu ya umuhimu wa muda katika huduma ya baada ya tukio la ubakaji. Kampeni hiyo inaendelea kupanuka kupitia washirika wake 11 duniani na machapisho yaliyo katika lugha nne tofauti. Mnamo mwaka 2017, TFG ilifanya kazi na vijana watetezi kutoka Kenya na Uganda kuandaa Kitini cha Kuwahusisha Vijana kaatika Kampeni ya EHM ("EHM Youth Engagement Toolkit" kwa Kiingereza).
- Kwa ujumla, ushirika wa TFG una wafuasi wa mtandao wa twitter zaidi ya milioni 13 kutoka nchi zaidi ya 50.
- TFG na washirika wake wamefaulu kutetea uingizwaji wa VAC na VAW kuwa moja ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals, "SDGs" kwa Kiingereza).
- Ili kuongeza hamasa, kutafuta ufumbuzi na kupaisha sauti za waanga wa ukatili, TFG ilisimamia matukio ya ngazi ya juu kwa nyakati maalum, ikiwemo kikao cha Baraza kuu la Umoja wa Mataifa, Tume ya Kusimamia Ustawi na Hadhi ya Wanawake, Siku ya Kimataifa ya Msichana na Kikao cha Women Deliver.

UNGANA NASI

Pamoja, tunaweza kuumba ulimwengu ambamo kila mtoto na kijana atakuwa salama, mwenye ulinzi na mwenye kustawi.
Kujifunza mengi kuhusu Together for Girls, tembelea togetherforgirls.org, Tufuatilie @Together4Girls au tutumie barua pepe: info@togetherforgirls.org.